Mwongozo wa Familia wa Kujifunza

Muhtasari wa yale watoto wanastahili kufahamu na kuweza kufanya na njia za familia kuongeza masomo nyumbani.

“Tunaamini familia ni wenzetu. Niwa kwanza na waelimishaji wa watoto wenye nguvu zaidi . Pamoja tutahakikisha mafanikio ya wanafunzi wote.”

- Mrakibu Emmanuel Caulk,
Shule za umma za kata ya Fayette

Kuhusu mwongozo wetu wa kujifunza:

Mwongozo huu unawakilisha baadhi ya vitu muhimu mtoto wako anapaswa kujua na kuweza kufanya kufikia MWISHO wa mwaka wa shule katika usanaa wa lugha ya Kiingereza (ELA) na Hesabu. Malengo ya kujifunza inasaidia familia na walimu kujua lini wanafunzi wanahitaji msaada zaidi na lini wanahitaji changamoto zaidi.

Familia zinaweza kufanya nini?

Kuna mengi ya kufanya kumsaidia mtoto wako kujifunza na kusaidia kuwatayarisha kwa maisha yao ya mbeleni. Haya ni mambo machache ambayo yatawasaidia wanafunzi kufanikiwa:

1. Eleza na mtoto wako jinsi masomo yalivyo muhimu kwako. Waeleze elimu inastahili, kwamba ni msingi wa mafanikio.
2. Fanya shule iwe kipaumbele kwa kumpeleka mtoto wako shuleni kwa wakati kila siku. Kwa kufanya hivyo unaonyesha kwamba ni kipaumbele.
3. Shirikiana na shule kujenga kuheshimiana.
4. Himiza uhuru; ruhusu watoto wako wafanye makosa na wakubali wajibu wa chaguo lao.
5. Jadiliana na mtoto wako kuhusu nini kinatendeka shuleni.
6. Wasiliana mara kwa mara na walimu wa mtoto wako kuhakikisha mtoto wako anafanya maendeleo kwa mwaka mzima.
7. Hudhuria mikutano ya mzazi-mwalimu na shughuli zingine za shule inapowezekana.
8. Una haki ya kujua jinsi mtoto wako anavyoendelea; usisite kuwasiliana na mwalimu wake kama una mswali.

Kuzungumza na Mwalimu wa Mtoto wako

Ni muhimu kuwasiliana na mwalimu wa mtoto wako na shule mara kwa mara kuhusu maendeleo ya mtoto wako kuhusu malengo ya masomo. Hapa kuna mifano ya maswali ya kuuliza:

- Mtoto wangu ana nguvu wapi na ni wapi anahitaji kuboresha?
- Maendeleo ya mtoto wangu yanapimwa vipi katika mwaka mzima?
- Naweza kuona mifano ya kazi za mtoto wangu? Vipi wanafikia ama hawafikii malengo ya masomo?
- Mtoto wangu yuko njiani kufikia malengo ya kiwango cha darasa? Kama sivyo, misaada gani shule itatoa? Naweza kufanya nini nyumbani?
- Mtoto wangu yuko kwa ama juu ya matarajio ya masomo? Kama ndivyo, nini kingine shule inaweza kutoa? Naweza kufanya nini nyumbani?
- Umesoma IEP ya mtoto wangu? Ni makao gapi yanayofanyiwa mtoto wangu?
- Mtoto wangu anajifnuza Kiingereza. Kukua kwa lugha ya mtoto wangu kunasaidiwa vipi shuleni?

Kuzungumza na Mtoto wako

Hii inasikika kama kawaida?
“Shule ilikuwaje leo?”
“Sawa”
“Ulifanya nini?”
“Hakuna”
Hiyo ni sawa, endelea kuuliza!

Wanafunzi ambao wazazi wao wanazungumza nao kuhusu shule hufanya vizuri kimasomo katika shule. Hapa kuna njia unaweza kumhusisha mtoto wako na usaidie mafaniko yao:

- Teua wakati kila siku kuzungumza na mtoto wako kuhusu shule.
- Uliza mtoto wako akueleze jambo moja walisoma leo. Nini mtoto wako anafaikiri kuwa inavutia sana? Nini inaonekana ngumu?
- Tizama ama pitia makaratasi na miradi ambayo mtoto wako analeta nyumbani kutoka shuleni. Uliza mtoto wako: unajuaje hivo? Unadhani nini? Unatambua nini? Kwa nini uliifanya vile ama hivi? Kuna njia nyingine ya kupata jawabu hilo?
- Pongeza mtoto wako kwa kazi ngumu na bidii, sio tu kwa “majibu sahihi”.
- Uliza maswali kuhusu mtoto wako anafikiria nini: Unajuaje? Unafikiri nini? Unatambua nini? Uliifanya hivyo kwa nini? Kuna njia nyingine ya kupata jawabu hilo?

Kusaidia kujifunza mbali na shuleni

Kujifunza hakusimami wakati wanafunzi wanatoka shuleni. Hapa kuna njia ambazo unaweza kusaidia kujifunza nje ya darasani:

- Somea mtoto wako, soma na mtoto wako, na uhimize wakati wa familia wa kusoma—katika lugha ambayo unajisikia starehe.
- Tengeneza mahali patulivu na starehe na uunde ratiba ya kila mara kwa wanafunzi wako kufanya kazi za shuleni za kufanyia nyumbani ama shughuli nyingine.
- Hakikisha wewe na mtoto wako mko na kadi ya maktaba na mnahudhuria shughuli za kusoma kwa familia nzima.
- Jaribu kuanzisha ratiba ya mara kwa mara ya kufanya homework ama shughuli zingine za kujifunza.
- Tumia mwongozo huu kulenga malengo machache ya kujifunza, jaribu maoni kadha ya kujifunza nyumbani.

Nini mwanafunzi wako anapaswa kujua na kuweza kufanya katika sanaa ya Lugha ya Kiingereza (ELA):

Lugha

- Kupitia kusoma na mazungumzo, pata na utumie misamiati mizuri migumu na maneno ya hali ya juu kama busara, furahisha na isiyo shiriki.
- Wakati wa mazungumo, anapaswa kuuliza maswali, kusikiza kwa maoni ya wengine, na kuchangia maoni ama mawazo yako mwenyewe kulingana na uzoefu wa kibinafsi wa yale amejifunza kwa kusoma ama kwa vyombo vingine.

Kusoma na fasihi

- Tambua mawazo muhimu na maelezo ya kusaidia katika kitabu chenye hadithi ya ukweli.
- Tambua mandhari (yaani, urafiki, huzuni/kufiwa ama kupoteza, mtu dhidi ya hali ya asili, hekima) ama funzo katika hadithi, hadithi zilizotungwa, na shairi ambayo anaisoma.
- Fanya mawazo (“soma kwa kina” kuunda maoni) kuhusu wahusika katika kitabu kutokana na mawazo ya wahusika, maneno, na vitendo.
- Shauriana na kamusi ili kufafanua maana ya maneno.

Kuandika

- Andika maelezo mafupi ama maoni ya hadithi na utumie maelezo ya kina kutoka kwenye maandishi kuyaunga mkono mawazo yako.
- Andika muhtasari mfupi kwa maneno yako mwenyewe ya habari ulizozikusanya kupitia utafiti.
- Andika kuhusu tukio ukitumia mwelekeo sahihi na mealezo ya kusaidia.
- Andika katika herufi ama maneno sahihi.

Jinsi ya kuhimiza mafunzo ya ELA nyumbani

- Fanya kusoma kuwe sehemu ya kawaida ya kila siku.
- Zungumza kuhusu vitabu ambavyo mtoto wako anasoma. Nini amejifunza kutoka kwa vitabu vyenye hadithi ya ukweli ama makala? Baada ya kusoma kitabu ama hadithi ya kutunga, uliza mtoto wako aseme ni vipi mhusika mkuu alibadilika kwa kitabu na kwa nini?
- Tengeneza “sanduku la misamiati” la familia na uhimize jamii nzima kusikiza na kutafuta maneno mapya ya kuongezea. Mara neno lipo katika sanduku, kila mmoja anakiwa atafute nafasi ya kulitumia katika mazungumzo ya kila siku. Ifanye iwe mchezo na mpe kila mmoja alama kila wakati wanapotumia mojawapo ya maneno hayo.
- Himiza watoto wako kuandika kila siku. Wafanye waandike barua pepe ama waandike barua kwa familia na marafiki kueleza mafanikio maalum ama matukio ya kusisimua. Mtoto wako anaweza weka jarida la uzoefu na matukio mageni.

Tafadhali ungana na mwalimu wa mtoto wako na uulize kuhusu rasilimali za masomo ya nyumbani zinazohusika na programu za kipekee za kusoma na kuandika.

Nini mwanafunzi wako anahitaji kufahamu na kuweza kufanya katika hesabu:

- Fikiri kuhusu na tatua hesabu za maneno ukitumia kuongeza, kuondoa, kuzidisha na kugawanya.
- Elewa uhusiano baina ya kuzidisha na kugawanya.
- Chora mfano ama picha kuonyesha hesabu za kuzidisha ama kugawanya.
- Fahamu na utumie kuzidisha (hadi 10 x 10) kutatua matatizo.
- Tumia mbinu mbali mbali kuongeza na kuondoa ndani ya 1000.
- Tofautisha na uwakilishe fraksheni za kawaida, kama vile ½, 1/3, ¼, 1/6 na 1/8 kama sehemu sawa za nzima (1/2 ya rektango) na sehemu sawa ya kikundi (1/3 ya biskuti 12 ni kuti 4).
- Linganisha fraksheni. Kwa mfano: ipi kubwa: ¼ ama 1/3?
- Tofautisha hali ya miundo kuitaja na kuianisha. Kwa mfano: Nini inafanya pembe tatu kuwa pembe tatu?
- Amua mviringo (umbali wa mzunguko wa muundo wa kona mbili katika kitengo mraba) na ya ukubwa wa nafasi katika muundo wenye kona mbili ambayo imepimwa katika kitengo mraba) ya miundo na ziweke alama ya kitengo sawa ya kitengo cha mapimo, kama vile fiti ama fiti mraba.
- Kusanya, wakilisha, eleza, na ufafanue data, kama vile kuhusu mahali ambapo wanafunzi wanapenda kula ama kutembelea. Weka data katika grafu.
- Pima na ukadirie musa, uzito na kiasi cha uoefu ama majimaji, na utatue hesabu ya maneno inayohusiana na kiasi.
- Tafuta eneo la miundo na unganisha eneo kwa kuzidisha na kuongeza.

Jinsi ya Kuhimiza Mafunzo ya Hesabu Nyumbani

- Ukiwa dukani, ambia mtoto wako akadirie jumla ya gharama ya manunuzi. Unapokuwa unalipa, unaweza pia kuuliza, “Tutarudishiwa pesa ngapi?”

- Uliza mtoto wako kutumia kuzidisha na kugawanya katika hali ya kila siku. Kwa mfano: “Ukiona ndege watano, je kuna mabawa ngapi? Ukigawana biskuti dazeni moja katikati kati ya watu wanne, Je, kila mmoja atapata biskuti ngapi?”

- Pamoja na mtoto wako, rekodi hali ya joto ya Lexington kila siku kwa wiki moja. Uliza mtoto wako atengeneze grafu kuonyesha mabadiliko ya joto.

- Fanya mazoezi ya kuhesabu na kuruka (kuhesabu kuelekea mbele ama kurudi nyuma kwa nambari mbali na 1) kila siku kusaidia wanafunzi kujifunza kuzidisha. Kwa mfano, hesabu ukiruka kwa 4 = 4, 8, 12, 16, na kadhalika.

Tafadhali ungana na mwalimu wa mtoto wako na uulize kuhusu rasilimali za masomo ya nyumbani zinazohusika na programu za kipekee za hesabu.

FAYETTE COUNTY PUBLIC SCHOOLS
1126 Russell Cave Road
Lexington, KY 40505

859-381-4100
www.fcps.net

Brosha hii imechapishwa na shule za umma za kata ya fayette.

Ilitengenezwa Fall 2016